

TANGAZO LA SERIKALI NA. \_\_\_\_\_ la tarehe \_\_\_\_\_

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA)

(SURA YA 287)

**SHERIA NDOGO**

Zimetungwa chini ya kifungu cha 153

**SHERIA NDOGO ZA (KIBALI CHA UJENZI) HALMASHAURI YA  
WILAYA YA IRINGA, 2017**

Jina na mwanzo wa kutumika 1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Kibali cha ujenzi) Halmashauri ya Wilaya ya Iringa za mwaka, 2017 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali.

Matumizi 2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika maeneo yote Ndani ya Halmashauri.

Tafsiri 3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa pale itakapoelezwa vinginevyo:-

‘Afisa mwidhiniwa’ maana yake ni Mhandisi wa Ujenzi, Afisa Mipango Miji, Msanifu Majengo au Afisa yeyote wa Halmashauri anayehusika na masuala ya Ujenzi /ardhi, au afisa yeyote wa Halmashauri atakayeteuliwa na Mkurugenzi kusimamia sheria ndogo hizi.

‘Halmashauri’ maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Iringa.

‘Jengo’ maana yake ni nyumba ya kuishi, biashara, ofisi au itayotumika kwa shughuli nyinginezo zinazofanana na hizo iwe imekamilika kujengwa au la, iliyojengwa kwa mawe,

matofali, matofali ya sementi na ambayo imezekwa kwa bati, vigae au “asbestos”.

‘Kibali’ maana yake ni ruhusa au idhini itakayotolewa na Halmashauri kuruhusu ujenzi wa jenge lolote katika Halmashauri.

‘Maeneo maalum’ maana yake ni pamoja na maeneo ya Ifunda, kidamali, Tungamalenga, Magozi, Itunundu, Kimande, Mbuyuni, Mboliboli, Migoli, Isman Tarafani na maeneo yote yatakayangazwa na Halmashauri kuwa maeneo maalumu.

‘Mkurugenzi’ maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Iringa pamoja na Afisa yeyote atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi.

Maombi ya kibali 4. (1) Mtu yeyote anayetaka kujenga jengo la aina yoyote katika maeneo maalum atatakiwa kuomba na kupata kibali cha ujenzi kutoka Halmashauri.

(2) Maombi ya kibali cha ujenzi yataambatanishwa na Ramani ya jengo iliyochorwa na mtaalam anayetambuliwa kisheria.

Masharti ya kibali 5. (1) Kibali kitatolewa baada ya mwombaji kutimiza mambo yafuatayo:-

- (a) Amewasilisha michoro ya ramani ya jengo
- (b) Awe amelipa ada ya ukaguzi wa ramani
- (c) Awe ana kiwanja au eneo linalotambulika ambalo anatakiwa kujenga jengo hilo.
- (d) Awe amelipia ada ya ardhi kwa viwanja vilivyopimwa

(2) Ramani zitakazowasilishwa Halmashauri zitatakiwa kuwa na vipimo vitakavyokubaliwa na Afisa Mwidhiniwa.

(3) Kibali kitatolewa baada ya mwombaji kutimiza masharti yaliyotajwa katika Sheria Ndogo hizi na

baada ya ramani kukaguliwa na kupitishwa na Afisa Ardhi, Mhandisi wa Ujenzi, Afisa Afya na Afisa Mpango Miji.

Muda 6. (1) Mwombaji atakiwa kuanza ujenzi katika muda wa siku  
wa  
ujenzi tisini (90) kuanzia tarehe ya kupewa kibali.

(2) Mtu yeyote atakayeanza shughuli ya ujenzi bila ya kuwa na kibali atakuwa ametenda kosa katika sheria ndogo hizi

Wajibu 7. (1) Afisa Mwidhiniwa anaweza wakati wowote wa kazi  
wa  
Afisa kuingia katika eneo lolote ambalo ujenzi unafanyika kwa madhumuni ya kufanya ukaguzi wa shughuli za ujenzi.

Mwidhiniwa

(2) Endapo Afisa Mwidhiniwa atabaini kuwa ujenzi unaofanyika hauna kibali au Mjenzi anajenga jengo hilo kinyume na masharti ya kibali na kinyume cha ramani iliyoidhinishwa na Halmashauri, Halmashauri itatoa Notisi ya kusimamisha ujenzi au kubomoa jengo hilo katika muda utakaooneshwa katika Notisi hiyo.

kukataliwa 8. (1) Halmashauri inaweza kukataa kupitisha ramani  
kibali endapo:-

- (a) Ujenzi unaokusudiwa kufanywa unavunja Sheria, Kanuni na Taratibu za ujenzi,
- (b) Ramani zilizowasilishwa hazikidhi masharti ya ujenzi,
- (c) Itabainika kuwa mwombaji sio mmiliki halali wa kiwanja au eneo ambalo jengo linakusudiwa kujengwa,

(2) Bila kuathiri masharti ya Sheria Ndogo hizi ujenzi wa majengo ya Serikali hautahitajika kulipia ada ya kibali .

makosa 9. Mtu yeyote atakayevunja au kushindwa kutekeleza  
na  
adhabu masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi shilingi elfu hamsini (50,000/=) au kifungo kisichozi miezi kumi na mbili au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo.

Mhuri wa Halmashauri ya Wilaya ya Iringa umebandikwa katika sheria ndogo hizi kufuatia mkutano wa baraza la madiwani uliofanyika tarehe.....mwezi.....201.. mbele ya ;

.....  
ROBERT MASUNYA  
MKURUGENZI MTENDAJI HALMASHAURI YA WILAYA YA IRINGA.

.....  
STEPHEN MHAPA  
MWENYEKITI HALMASHAURI YA WILAYA YA IRINGA.

NAKUBALI

.....  
MHE. GEORGE B.SIMBACHAWENE (MB)  
WAZIRI WA NCHI –OR-TAMISEMI

DODOMA,

TAREHE.....MWEZI.....2017.